



Baraza la Wakimbizi la Scotland (scottish refugee council)

Habari kwa wanaotafuta hifadhi wanaoishi katika makazi ya dharura

Ukijihisi vibaya muda mfupi tu baada ya kuwasili nchini humu, utakuwa na shida kumwona daktari upesi. Ikiwa una maumivu madogomadogo utamwona mkemia au mtaalamu wa madawa ya wanadamu akushauri au piga simu ya kuomba msaada kutoka kwa idara ya matibabu ya NHS 24.

NHS 24

Ukijihisi vibaya au ukihitaji habari za kiafya unaweza kupiga simu kwa NHS 24 (Simu: 0845 4 242424). Simu hii utapiga bure kupata ushauri bila malipo kutoka kwa muuguzi. Muuguzi kwenye simu atakushauri unachopaswa kufanya na hali yako ya kiafya ilivyo.

Mfamasia

Wataalamu wa madawa au wafamasia ni wataalamu wa kiafya ambao watakupa madawa uliyoandikiwa na daktari wa mwili kwa ujumla au meno. Watakushauri pia juu ya magonjwa ya kawaida. Iwapo unasaidiwa na Serikali kifedha au ijulikanavyo kama Income Support au una Cheti cha HC2 una haki ya kupata matibabu ya bure. Unapaswa kuingia tu katika duka la madawa na kuuliza ushauri. Jamii nyingi zina maduka yao yanayojulikana katika maeneo yao.

Daktari

Nchini Uingereza Daktari hutoa huduma ya kwanza ya kiafya kwa jamii zilizo karibu. Huduma ya madaktari wa familia hutolewa bure kwa wakimbizi na kwa wanoomba hifadhi. Madaktari wanaotoa huduma hii wanajulikana kama General Practitioners au kwa ufupi GP. Yule GP wako ndiye anayepaswa kuwa mtu wa kwanza kumwona iwapo wewe au mtu ye yote katika familia yako anajihisi vibaya au amepata majeraha madogomadogo. Baraza la Wakimbizi la Scotland litaandikia idara ya afya kwa niaba yako likiomba usajiliwe na GP aliye karibu nawe. Baada ya siku chache bila shaka utapokea barua katika anwani yako itakayokuwa na maelezo kamili kumhusu GP aliye karibu. Ni muhimu sana kwako kujisajili kwa GP mara tu unapowasili kwa sababu ni kupitia tu kwa daktari huyu ambapo utapata huduma nyingi za kiafya.

Dharura

Ukipatwa na ajali au ugonjwa mkali nenda katika idara ya ajali na dharura ya hospitali iliyo karibu nawe. Hii ni huduma inayotolewa bure kwa kila mtu. Iwapo u mgonjwa sana hivi kwamba hauwezi kufika hospitalini unapaswa kupiga simu nambari 999 ili gari la wagonjwa, ambulansi, likupeleke hospitalini. Idara ya dharura hufunguliwa usiku na mchana. Ikiwa hali yako ina umuhimu wa hali ya juu utashughulikiwa mara moja. Katika hali zingine zote taarifa inayokuhusu itachukuliwa kikamilifu na itakubidi usubiri kwa masaa kadhaa kabla ya kuonana na daktari.